

TANGAZO

MSAADA WA MIRADI YA MAENDELEO KWA JAMII ZA WAFUGAJI

Tangazo linatolewa kwamba, jamii za wafugaji kwa kupitia mashirika yao yaliyosajiliwa (NGOs, CBOs, FBOs) wanakaribishwa kuomba misaada ya maendeleo kwa miradi ifuatayo:

1. Utunzaji wa misitu iliyo katika vijiji vyao;
2. Miradi ya mabwawa ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo;
3. Uandishi na usambazaji wa vitabu kuhusu njia za asili za uhifadhi wa misitu, mazingira na vyanzo vya maji;
4. Michakato ya upatikanaji wa Hati za ki-kimila kwa maeneo yanayokaliwa na jamii za wafugaji; na
5. Maendeleo ya miradi ya mashamba ya malisho ya mifugo.

Maombi haya yasizidi shilingi milioni sabini na tano (75,000,000 Tshs), na yapitie kwa Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri ambako hizo jamii za wafugaji zipo. Maombi hayo yatumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji
Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF)
S.L.P 15605

Arusha

Kwa mawasiliano zaidi: 0652468219

Mwisho wa kutuma maombi ni Ijumaa, tarehe 19 Februari, 2021.